



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MUDA KWA WATUMISHI WA
UMMA YA KUANDIKISHA NA KUANDAA ORODHA YA WAPIGA KURA
KATIKA MITAA KWA AJLI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA
WA NOVEMBA 2024

Kwa madhumuni ya kuandaa Orodha ya Wapiga Kura katika Mitaa, na kwa kuzingatia Kanuni ya 10 (2) ya *Kanuni za Uchaguzi wa Wenyeviti wa Mitaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji Tangazo la Serikali Na.574 la tarehe 12/7/2024*, Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela anatangaza nafasi za kazi za muda kwa Watumishi wa Umma watakaoandikisha na kuandaa Orodha ya Wapiga Kura katika Mitaa kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Novemba 2024.

SIFA ZA MWOMBAJI

- (a) Awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi.
- (b) Awe ni mtumishi wa umma mwenye elimu ya kidato cha nne au zaidi na anaejua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
- (c) Awe muadilifu na muaminifu.

- (d) Asiwe mtumishi wa kada ya Mtendaji wa Mtaa au Mtendaji wa Kata.
- (e) Asiwe kiongozi au kada wa Chama cha Siasa.

MASHARTI YA JUMLA

- (i). Mwombaji lazima aainishe Mtaa anaomba kufanyia kazi
- (ii). Mwombaji aambatishe:-
- (a) Nakala za vyeti vya elimu au taaluma.
 - (b) Wasifu (CV) ukionesha anuani yake ya makazi, namba za simu za kuaminika.
 - (c) Picha 2 zenye ukubwa sawa na picha iliyomo kwenye pasi ya kusafiria (Passport size) za hivi karibuni.
- (iii). Barua za maombi zipitie kwa mwajiri wa mtumishi.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:-

Msimamizi wa Uchaguzi,
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela,
200 Barabara ya Buswelu,
S.L.P 735
33822 MWANZA.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 23 SEPTEMBER 2024

Limetolewa na :-

Umy Mohamed Wayayu,
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
MWANZA
16 SEPTEMBER 2024

